**SERIKALI YA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS- TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**(OR-TAMISEMI)**

**WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA (TARURA)**

**NA**

**WAKALA WA BARABARA TANZANIA (TANROADS)**

# PROGRAMU YA MAENDELEO YA BARABARA KWA USHIRIKISHAJI WA JAMII NA UFUNGUAJI WA FURSA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI (RISE) (P164920)

# RASIMU YA MWONGOZO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MASUALA YA KIJAMII (ESMF)

**DECEMBER, 2020**

## MUHTASARI WA KIUTENDAJI

## UTANGULIZI

Serikali ya Tanzania, kupitia kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Wakala wa Barabara nchini Tanzania (TANROADS) inaandaa "Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi" (kuanzia sasa utajulikana kama Programu ya Maendeleo ya Barabara) inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Lengo Programu hii ni "Kuboresha upatikanaji wa bababara vijijini na kutoa fursa za ajira kwa wananchi katika maeneo ya vijijini yaliyochaguliwa na kujenga uwezo katika usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kujumuisha mbinu za ushirikishwaji wa jamii" kwa kuzipandisha hadhi na kuzikarabati.

Hivi sasa, Tanzania haina mtandao mzuri wa barabara zilizounganishwa na maeneo ya vijijini. Matokeo yake, fursa za maendeleo vijijini zinazorota. Kipimo cha ufikikaji vijijini nchini Tanzania ni 24.6% ikilinganishwa na nchi nyingine za Afrika Mashariki, yaani Kenya yenye 56% na Uganda 53%. Matokeo chanya yanayotokana na utekelezaji wa Programu hii ni ya muhimu katika kufungua fursa za kiuchumi katika maeneo ya vijijini. Fursa hizo zitaongozwa na falsafa ya "Usanifu wa Barabara Unaozingatia Mahitaji ya Watu" ambao unahakikisha kwamba mfumo mpya wa barabara za Tanzania unaundwa kwa kuzingatia mahitaji ya watu.

Programu ya Maendeleo ya Barabara unahusisha vipengele vinne: Ujenzi na Ukarabati wa Barabara za Vijijini; Uimarishaji wa Taasisi, Rasilimali Watu na Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi; Uhusishwaji, Ushirikishwaji na Usalama wa Jamii, na Ushughulikiaji Matukio ya Dharura.

## MWONGOZO WA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA MASUALA YA KIJAMII

Kwa kuwa eneo lengwa na usanifu wa miradi mikubwa na midogo ya Programu hii haifahamiki, na aina za miradi inayowezekana zimeelezwa kwa uwazi, Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESMF) umeandaliwa. Mwongozo huu unaanzisha mchakato, na kubainisha dhima na majukumu ya kushughulikia masuala ya kimazingira na ya kijamii katika miradi mikubwa na midogo kuanzia kwenye maandalizi, upitiaji na uidhinishaji, hadi katika hatua za utekelezaji wake. Mwongozo huo unatoa maelekezo kwa watekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara, kubainisha na kupunguza vihatarishi vinavyoweza kujitokeza pamoja na athari za kimazingira na za kijamii katika hatua zote za utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara, kama vile upangaji, usanifu, utekelezaji, uendeshaji pamoja na hatua zote za kuukamilisha Mpango huu, na miradi mingine mikubwa na midogomidogo.

## Mwongozo wa Kisheria na Kitaasisi Unaoongoza Utekelezaji wa Mwongozo Huu

Mwongozo huu unawasilisha taratibu za wazi, jumuishi, na dhahiri zinazoendana na sheria za Tanzania na zile za Mazingira na Jamii za Benki ya Dunia, hususani vigezo kumi vya kimazingira na kijamii. Mwongozo huu utaongozwa na Sera za Taifa pamoja na mwongozo wa kisheria na kitaasisi, na Miongozo ya Benki ya Dunia ya Kimazingira na Masuala ya Kijamii.

Baadhi ya sera za Serikali ya Tanzania ambazo zitaongoza utekelezaji wa Mwongozo huu wakati wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara zitahusisha: Sera ya Taifa ya Mazingira (1997); Sera ya Taifa ya Jinsia (2002); Mkakati wa Kuondoa Umasikini na Kukuza Uchumi Tanzania (MKUKUTA) II (2015) na Sera ya Taifa ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi ya mwaka 2010. Miongozo ya Taifa ya kisheria itakayoongoza utekelezaji wa Mwongozo huu wa Jamii na Mazingira ni: Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004; Sheria ya Barabara ya mwaka 2007; Sheria ya Ardhi ya mwaka 1999; na Sheria ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Na. 5 ya mwaka 2003. Kanuni na miongozo mingine muhimu katika utekelezaji wa Mwongozo huu inahusisha Kanuni za Tathmini na Ukaguzi wa Athari za Mazingira za mwaka 2005 na marekebisho yake ya mwaka 2018; Kanuni za Usimamizi wa Barabara za mwaka 2009; Viwango Mahususi vya Ujenzi wa Barabara vya mwaka 2000; na Kanuni za Mazingira za Utendaji katika Ujenzi wa Barabara nchini Tanzania (Wizara ya Miundombinu, 2009).

Mwongozo wa kitaasisi kuhusu vigezo vya kiutawala na mipangilio ya kitaasisi katika utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara umeidhinishwa kikamilifu katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira (EMA) Na. 20 ya mwaka 2004 na kwamba Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) na Kitengo cha Mazingira (DoE) ni taasisi kuu zenye majukumu ya usimamizi wa masuala ya mazingira nchini Tanzania. Taasisi nyingine zilizopewa majukumu hayo ni: Kamati ya Taifa ya Ushauri wa Mazingira; Waziri mwenye Dhamana ya Mazingira; Mkurugenzi wa Mazingira; Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira; Sekta za Wizara; Sekretarieti za Mikoa; Mamlaka za Serikali za Mitaa (Jiji, Manispaa, Wilaya, Mji, Kata, Kijiji, Mtaa na Kitongoji).

Hata hivyo, sheria zilizounda Wakala zinazoshughulikia utekelezaji, yaani TARURA na TANROADS, zimezipa Wakala hizo majukumu ya kushughulikia masuala ya kimazingira na kijamii, hasa katika sekta ya barabara. Kufanya hivyo kutasaidia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara. Wakala hizo zitaunda Kamati ya Utendaji ambayo itaafikiana na uamuzi unaohusiana na utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara.

## Mwongozo wa Benki ya Dunia wa Mazingira na Masuala ya Kijamii

Malengo ya Mwongozo wa Benki ya Dunia wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESF) ni kuwalinda watu pamoja na mazingira dhidi ya athari mbaya zinazoweza kujitokeza kutokana na miradi inayofadhiliwa na Benki hiyo na kuhamasisha maendeleo endelevu.

Mwongozo huu wa Mazingira unahusisha mambo mengi ikiwa ni pamoja na maboresho muhimu katika uwajibikaji, uwazi, kutokuwa na ubaguzi, ushirikishwaji wa jamii, ushiriki na uwajibikaji wa umma. Pia Mwongozo huu unaweka msisitizo wa serikali inayokopa kujijengea uwezo binafsi wa kushughulikia vihatarishi vya kimazingira na kijamii, na athari zinazotokana na utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na maendeleo.

Mwongozo huu unahusisha masuala yafuatayo: Dira ya Benki ya Dunia inayohusu Maendeleo Endelevu; Sera ya Benki ya Dunia ya Mazingira na Masuala ya Kijamii katika Kufadhili Uwekezaji wa Miradi ambayo inaweka bayana vigezo vinavyotakiwa wakati wa kupeleka maombi katika Benki hiyo; Viwango 10 vya Kimazingira na Kijamii (ESSs) ambavyo vinaweka bayana vigezo vya wakopaji wanaotaka kutuma maombi; Maelekezo ya Benki: Maelekezo kuhusu mazingira na Masuala ya kijamii kwa ajili ya Ufadhili wa Uwekezaji wa Miradi; na Maelekezo ya Benki kuhusu Ushughulikiaji wa Vihatarishi na Athari kwa Watu au Makundi yaliyo katika Hali Hatarishi; na Miongozo ya Benki ya Dunia inayohusu Mazingira, Afya na Usalama (EHSGs).

Viwango hivyo vya Benki ya Dunia vya Kimazingira na Kijamii (ESSs) ni: Kiwango Na. 1 - Tathmini na Usimamizi wa Vihatarishi na Athari za Kimazingira na Kijamii; Kiwango Na. 2- Wafanyakazi na Mazingira ya Kazi; Kiwango Na. 3- Utoshelevu wa Rasilimali, na Usimamizi na Uzuiaji wa Uchafuzi wa Mazingira; Kiwango Na. 4 - Afya na Usalama wa Jamii; Kiwango Na. 5 - Upataji wa Ardhi, Mipaka ya Matumizi ya Ardhi na Uhamaji wa bila Kukusudia; Kiwango Na. 6 - Uhifadhi wa Bayoanuai na Usimamiaji Endelevu wa Rasilimali Asilia za Viumbe Hai; Kiwango Na. 7- Jamii za Kijadi / Kiafrika zinazopatikana Kusini mwa Jangwa la Sahara / ambazo Kihistoria hazijapewa huduma zinazostahili; Kiwango Na. 8 - Urithi wa Kiutamaduni; Kiwango Na. 9 - Usimamizi wa Fedha; na Kiwango Na. 10- Ushirikishaji wa Wadau na Utoaji wa Taarifa. Katika Mwongozo huo, Kiwango nambari 9 sio muhimu kwa Programu ya maendeleo ya Barabara.

Kulingana na Kiwango nambari 10, ushauri uliombwa kutoka kwa wadau wanaohusika wakati wa maandalizi ya Mwongozo huu na nyaraka nyingine za miongozo (kwa mfano, SEP, VGPF, LMP, RPF, ESCP). Wakopaji waliandaa warsha ya wazi ya ushauri mnamo tarehe 9 Januari, 2020 kwa ajili ya nyaraka zinazohusu miongozo (Tazama Kiambatisho X chenye orodha ya wadau ambao waliombwa ushauri). Mrejesho kutokana na warsha inayohusu ushauri umeingizwa katika nyaraka za miongozo mbalimbali.

## TARATIBU ZA KIMAZINGIRA NA MASUALA YA KIJAMII

Sio tu kwamba Mwongozo huu unabainisha vihatarishi na athari za kimazingira na kijamii zinazoweza kujitokeza kutokana na ujenzi wa barabara ambazo zinatazamiwa kujitokeza wakati wa utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara, bali unafafanua michakato ya kimazingira na kijamii ambayo inahusisha mchujo wa miradi mikubwa na midogo, maandalizi ya vifaa, na mkakati wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Barabara.

Mchujo wa miradi mikubwa na midogo utahusisha kutenga miradi mikubwa/midogo ambayo imetimiza vigezo vilivyotolewa; azimio la kipimo cha vihatarishi vya kimazingira na kijamii na kueleza kiwango cha juhudi zinazohitajika.

Ikiwa mradi mkubwa/mdogo umepitia mchakato wa mchujo, maandalizi ya vifaa vya kimazingira na kijamii yatafanyika na kuhusisha Tathmini ya Athari za Kimazingira na Kijamii (ESIA), ESMP na kwa mujibu wa Sheria za Nchi, hakuna shughuli za ujenzi zitakazoanza katika eneo husika la mradi kabla ya uidhinishwaji wa NEMC kulingana na ripoti ya utafiti wa Tathmini ya Athari za Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESIA) na hivyo utoaji wa cheti kutoka kwa ESIA utafanyika.

Mkakati wa utekelezaji wa Mwongozo huu unahitaji ushirikishwaji kamili wa usimamizi wa masuala yanayohusu mazingira na jamii kama ambavyo yamehusishwa katika Mpango wa Usimamizi wa Masuala ya Kmazngira na Kijamii (ESMP) na kuingizwa katika nyaraka za zabuni na mikataba ya wakandarasi ili kuhakikisha utekelezaji kamilifu wa miradi mikubwa na midogo kama ilivyofafanuliwa katika Mpango wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii (ESMP). ESMP inaelekeza kwamba Mkandarasi aandae na kuwasilisha ESMP (tofauti na iliyowasilishwa katika ESIA) na kuzingatia wakati wa utekelezaji wa miradi mkubwa/miradi-midogo. Mwongozo huu utahakikisha kwamba ushauri wa wazi kwa wadau wote wa miradi mikubwa na midogo umetolewa na kuandikwa vizuri ili kuijulisha ESIA na usanifu wa miradi mikubwa na midogo. Hata hivyo, Mwongozo huu wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii utahakikisha kwamba Mkakati wa Ushughulikiaji Malalamiko unaandaliwa ili kupokea, kutathmini na kutatua malalamiko yote yanayohusiana na miradi mikubwa na midogo.

## HITIMISHO

Kwa kuhitimisha, Mwongozo wa Usimamizi wa Mazingira na Masuala ya Kijamii unaanzisha mchakato, na kufafanua dhima na majukumu ya kukabiliana na masuala ya kimazingira na kijamii kwa ajili ya Programu ya Maendeleo ya Barabara na kuelekeza kimkakati Programu hii katika hitimisho endelevu kwenye vipengele vya mazingira, kiuchumi na kijamii. Kwa pamoja, vipengele hivyo vimesisitizwa na Serikali ya Tanzania na Benki ya Dunia kama shirika linalotoa misaada.